

Uhuru Uk.16 Tarehe  
22/12/2020

# Wavuvi waonywa wasitumie zana haramu kuvua samaki ziwani

**NA BALTAZAR MASHAKA, Musoma**

OFISA Uvubi wa Halmashauri ya Musoma Vijijini, Augustine Costantine, amewataka wavuvi kujiepusha na uvubi haramu, badala yake wazingatie sheria, utaratibu na kanuni zinazosimamia uvubi wa rasilimali za Ziwa Victoria na kuzifanya endelevu.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki iliyota, baada ya viongozi wa serikali ya wilaya hiyo, mbunge na maofisa wa Benki ya Equity, kuwatemeblea wavuvi wa mialo ya Busekera, Bwai Kumsoma, Iriga na Lukuba.

Alisema ni muhimu wavuvi wakabadilika na kuzingatia sheria, utaratibu na kanuni ili kuachana na matumizi ya zana au nyavi haramu na kwamba kila mvuvi awe mlinzi na mwalimu wa mwenzake.

"Ndugu zangu wavuvi, umefika wakati

ninyi wenyewe mkomeshe uvubi haramu kwa kuzingatia na kutii sheria. Epukeni matumizi ya nyavi zisizoruhusiwa kisheria, ambazo zinatishia kutoweka kwa viumbi hai na samaki ndani ya Ziwa Victoria,» alisema Costantine.

Alisema halmashauri hiyo itaendelea kuwaelimisha wavuvi kwenye maeneo yote zinakofanyika shughuli za uvubi ili yaendelee kuwa salama na kuwataka wavuvi kutambua umuhimu wa elimu hiyo ili kuepuka kuvunja sheria na kuingia hatiani.

Katika hatua nyingine, vikundi 79 vya wavuvi vyenye wanachama 1,035 vya Wilaya ya Musoma Vijijini, vimeandikishwa kwa ajili ya kupewa mikopo kutoka katika taasisi za fedha.

Vikundi hivyo vya mialo ya Bwai Kumsoma, Busekera na visiwa vya Iriga na

22/12/2020

Sokoto ya Kitunguu imeshuka, ambapo kitunguu kimoja kinauzwa kati ya Sh 50 mpaka 100. (Picha na Alpha Nsemwa).

## Sikunge wazindua uogeshaji mifugo

Na Lucas Raphael,  
Tabora

**H**ALMASHAURI ya Wilaya ya Sikunge mkoani Tabora imezindua zoezi la uhamilishaji na uogeshaji mifugo.

Zoezi hilo litalofanyika katika kata zote 20 na vijiji 71 kwa lengo la kutokomeza magonjwa yaenezwayo na kupe na ndorobo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Tito Luchagula alisema zoezi hilo ni muhimu kwa kuwa litaokoa mifugo 371,000, yenye thamani ya Sh milioni 185.5.

Alisema zoezi hilo litagharimu Sh milioni 6.4 na litaongeza ubora wa

mifugo, uzito na maziwa yanayozalishwa wilayani humo.

Alisema zoezi hilo litawafikia wafugaji wote na litatekelezwa katika kata zote, zenye majosho ya kuogeshea mifugo.

Alibainisha kuwa wametengea Sh milioni 16 kwa ajili ya ujenzi wa majosho katika kata ambazo hazina miundombinu hiyo.

"Hii ni fursa muhimu kwa wafugaji, naomba kila mtu aichangamkie ili kuboresha zaidi mifugo yetu na kuongeza ubora, uzito na maziwa na hatimaye kuongeza vipato vyetu", alisema.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo, Mipawa Ma-

jebele aliishukuru serikali kwa kuwapatia dawa za ruzuku aina ya paranex lita 161.5 zenye thamani ya Sh milioni 6.4 kwa ajili ya kufanikisha zoezi hilo.

Alieleza kuwa wafugaji wilayani humo wamekuwa wakijipatia Sh bilioni 24.7 kwa mwaka kutokana na mauzo ya mifugo yao kwenye minada. Alisema halmashauri imekuwa ikipata Sh milioni 180 na serikali kuu Sh milioni 112.

Alikishukuru Kituo cha Uhamilishaji cha Taifa kilichopo Arusha (NAIC), kwa kuwapatia mbegu za ng'ombe 100. Mbegu hizo ni za ng'ombe wa nyama na maziwa.

Alitoa wito kwa

wakazi wa wilaya hiyo, kuunga mkono juhudzi za halmashauri hiyo katika kuboresha mifugo yao.

Mkuu wa wilaya hiyo, Peresi Magiri aliiitaka halmashauri hiyo kutekeleza kwa ufanisi mkubwa zoezi hilo ili kunufaisha wafugaji.

Aliitaka halmashauri kuahakikisha miundombinu inajengwa katika kila kata ili kufanikisha zoezi hilo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Rashid Magope aliiishukuru serikali kwa kufanya uzinduzi huo katika kata yake ya Tutuo. Alisema kuwa zoezi hilo ni muhimu, kwani litasaidia kuboresha mifugo yao.